# Our Voices — MULTILINGUAL

Majira ya Kipupwe 2021 | www.houstonisd.com/voices | Toleo la I Chapa ya 2


## UJUMBE KWA WAZAZI ...

# Maneno ya Olanga



**Kwenye upanda wa kulia wa Olanga kwenye picha, ni mamake, Bi. Bora ambaye anaendelea kukuza uhodari wake wa kushona. Dadake amekaa upande wake wa kushoto, huku anahudumia nchi yetu ndani ya National Guard (Walinzi wa Taifa) ya Marekani. Olanga kwa sasa amedumisha makini kwenye mafunzo yake ya kuwa Muuguzi Aliyesajiliwa.**

Familia ya Olashkoko inawakilisha mojawapo kati ya familia nyingi zilizohama hadi Marekani miaka mengi iliyopita. Tulikutana na Olanga, mtoto mmoja kati ya watano ambao pamoja na wazazi wake waliondoka kwao, Kongo, miaka misaba iliyopita ili kuanza safari yao hadi Marekani. Familia iliacha dada mkubwa, aliyeolewa na mama mwenye watoto watatu ambaye hakuweza kusafiri. Olanga anakumbuka jinsi ilivyokuwa vigumu kumuacha nyuma dadake; wanaendelea kuwasiliana lakini wana matumaini machache ya kukutana tena.

Kwa ajili ya vurugu na Vita vya Wenyewe kwa Wenyewe nchini Kongo, wazazi wake walifanya uamuzi wa kuondoka nyumbani na kuwatafutia maisha bora watoto wao. Walipitia miaka miwili migumu kwenye kambi za wakimbizi nchini Kenya. Kuhama kutoka nyumbani kwao nchini Kongo hadi kuishi kwenye tenti lilikuwa badiliko ambalo yeye na ndugu wake walikuwa hawajajitayarisha kukumbana nalo. Hali hizi ngumu, mazingira ya nusu jangwa ambapo mahema yao yalibebwa na mafuriko. Hali nchini Kenya hazikuruhusu kumea chakula chao wenyewe, vyakula kidogo vya kikebe tu ndivyo vilivyokuwa vinapatikana. Hapa ndipo mtunzi na baba yao, ambaye alikuwa mgonjwa, alizidi kugonjeka kiasi cha kuhitaji uangalizi wa kimatibabu.

Baada ya miaka miwili nchini Kenya, familia ilianza awamu ya pili ya ari yao ya kupata maisha bora jijini Nairobi. Huko, afya ya baba yao ikapata nafuu. Matumaini ya Familia ya Olashkoko ya kupata maisha nchini Marekani yaliendelea kuwa nao hadi walipofanya safari yao miaka 5 baadaye.

Leo, Olanga anaangazia viuri miaka mitatu ambapo yeye na familia yake wameishi nyumbani kwao kupya, Houston, Texas. Anabainisha shukrani zake kwa maisha mapya aliyo nayo sasa hapa Houston na pia usaidizi aliopokea kutoka kwa walimu wake kwenye Houston Independent School District.

Olanga aliulizwa kama anajuta chaguo la familia yake la kuja Marekani. Alisema, "Mwanzoni nilikuwa na maswali kuhusu kuja hapa. Ilikuwa tofauti kabisa. Tunaweza kujidumu hapa? Pindi tulipoishi hapa, hofu zote hizo zilififia. Kisha tukakutana na Bi. Shirin, alikuwa Kielelezo chetu. Aliisaidia familia yetu iwe kwenye njia sahihi."

Njia hiyo ilienda hadi dada mkubwa wa Olanga, Prista, akuhudumia nchi yetu kwenye Tawi la Jeshi la National Guard (Walinzi wa Taifa). Ari yake ya kufanya kazi hii ilianza alipoenda kwenye mojawapo kati ya kampasi zetu kuu, Westside HS.

Njia ya Olanga ilimuongoza kuelekea kazi kwenye taaluma ya kimatibabu kama Muuguzi Aliyesajiliwa. Ingawa anajishughulisha kwenye mafunzo yake, haachilii shabaha yake ya kuwa mchezaji densi wa kitaalamu. Anafafanua kwa bashasha jinsi angependa kuwa kwenye filamu na kucheza dansi. Kwa maneno yake mwenyewe, "Kila kitu kinawezekana. Mwenyezi Mungu bila shaka ana miujiza."

Mchakato wa uhamiaji wa Familia ya Olashkoko haukutokea bila matatizo. Wamevumilia na sasa familia imepanda daraja; babake amepona kikamilifu na anapokea mafunzo ya ukulima na Bi. Abora, mama wa Olanga, anaendelea kustawisha uhodari wake wa kushona, uhodari alioutoa nyumbani.


Alipoulizwa "Ungeshiriki nini na wengine ambao huenda ikawa wamehamia Marekani hivi karibuni?", Olanga anajibu kwa kutoa shukrani sana kwa shule, walimu na wilaya ambao waliinyoshea mkono yeye na familia yake. Anakaribisha wengine waje na ajizoeze badiliko kwa njia nzuri; ili kusoma kwenye shule murwa ambapo ukufunzi wa elimu unapatikana na wanafunzi wanaweza kufikia klabu za spoti, jamii, na familia kubwa inayojali.

Kwenye miaka mitatu iliyopita, Olanga amejifunza maadili shughulishi ya kazi. Kushiriki jinsi "kufanya kazi kwa bidii kunalipa; ukiingiza 100% kwa upole, unapokea 100% badili yake."

## KALENDA YA MITIHANI YA 2020–2021

Kalenda za mitihani za Texas Education Agency (Wakala ya Elimu ya Texas) zinapatikana ili kuhakikiwa. Maelezo ya kutahini ya STAAR/ STAAR Alt na TELPAS/ TELPAS Al inaweza kufikiwa kwa kubofya ***https://bit.ly/3psRRov***

## TONE LA BUSARA



Nicole Moore

Ninkuletea salamu kwa niaba ya Houston Independent School District (Wilaya Huria ya Shule ya Houston). Heri ya mwaka mpya! Mwaka wa 2021 unatupatia ahadi kuwa utakuwa mwaka murwa kwetu sote. Kutakuwa kuna mabadiliko kwenye ulimwengu tunaoishi. lakini jambo moja ambalo halitobadilika ni kuwa wanafunzi wetu WANAPEWA KIPAUMBELE. Kuna njia nyingi ambazo wazazi wanaweza kumsaidia mtoto wao afaulu.

Haya hapa mambo machache ambayo wazazi wanaweza kuyafanya ili kusaidia kufanikiwa kwa mtoto/watoto wao:

- Kumpatia mtoto wako sehemu kimya ya kazi ili mtoto wako asome, apokee mafunzo pepe, au afanye kazi za nyumbani za masomo. Watoto watadumisha makini zaidi wanapokuwa wana sehemu waliyoteuliwa ya kujifunza au kusoma.
- Kuunda maktaba ya nyumbani yenye vitabu, majarida, magazeti, komiki, n.k. Hii itamhimiza mtoto wako asome ambayo inaweza kusababisha mtoto wako awe mwandishi mzuri.
- Kuendelea kudumisha mawasiliano na mwalimu wa mtoto wako ili kuhakikisha kuwa amekamilisha kazi zote na kuwa anafaulu kwenye nyanja zote za masomo. Hii pia inaweza kufuatiliwa kwenye lango la HISD Parent Connect (Muunganisho wa Wazazi wa HISD) ***https://www.houstonisd.org/psc***
- Muhimu zaidi, jipatie muda wa kuingiliana na mtoto wako kuhusiana na shule, hii inaweza kuwa wakati wa chakula cha jioni cha kila siku ambapo watoto wanaweza kueleza kuhusu siku yao na wazazi wanaweza kuwa karibu na hisia au wasiwasi wa mtoto wao. Kuwapatia maneno ya kuwahimiza kila siku ili waendelee kuwa na motisha.
- Nyenzo nyingine murwa ni HISD@Home ***https://www.houstonisd.org/home***.

Tuzidishe muda tunaokuwa pamoja na watoto wetu. Waajiriwa wa shule na wasimamizi wa HISD wako tayari na wanapatikana ili kuwasaidia wazazi na wanafunzi. Tuifanye 2021 iwe mwaka murwa.

**Nicole Moore, Achieve 180 – Msimamizi wa Eneo**

## HISD | School Choice

HUNDREDS OF OPTIONS. ONE APPLICATION.

Kuwa mmojawapo kati ya wanafunzi wetu bora na wa hivi karibuni wa Magnet School (Shule za Magnet)! Peusha ufahamu na uhodari wako na sajili ili kujiunga na chaguo lako la shule za Magnet. Anzisha mchakato wa usajili leo kwa kuzuru ***https://www.houstonisd.org/enroll***

## TAREHE MUHIMU

**AWAMU YA 2: NOV. 7, 2020 – FEB. 26, 2021***

**AWAMU YA 3: FEB. 27, 2021**

*Tarehe ya mwisho ya wanafunzi wa sasa wa HISD ya kuwasilisha ombi la mahamisho

## MAELEZO YA NAULI YA WANAFUNZI YA METRO

Metro ni wakala kuu ya usafiri wa umma yenye makao yake makuu huko Houston, Texas. Inaendesha basi, reli hafifu, mpito upesi wa basi, njia za HOV na HOT, na huduma ya mpito mbadala jijini na kwenye sehemu nyingi za Kaunti ya Harris.

Ari ya METRO ni kutoa huduma salama, safi, zinazoaminika, na ingiliani za usafiri wa umma kwenye eneo letu.

### Maelezo ya Nauli ya Wanafunzi ya Metro

**Wanafunzi wa Chekechea hadi Darasa ya 12**

**Wanafunzi wa shule za kati na za upili wanaweza kulipa kwa pesa taslimu (kwenye basi pekee) na kupokea diskaunti ya asilimia 50 kwa kutumia kitambulisho chake cha mwanafunzi. Shule msingi pia zinaweza kulipa kwa pesa taslimu (kwenye basi pekee) bila kukubidi uonyeshe kitambulisho.**

### Student METRO Q® Fare Card (Kadi ya Nauli ya Mwanafunzi ya METRO Q®)

**Wanaweza kupata Student METRO Q® Fare Card au METRO Day Pass.**

**Utahitaji kitambulisho cha sasa cha shule, ratiba ya darasa, fomu ya uandikishaji, kadi ya ripoti (kwenye kijajuu cha barua za shule) au fomu ya usajili wa kadi ya nauli ya mwanafunzi ya METRO iliyotiwa saini na mzazi au mlezi**

Agiza kadi mtandaoni au chapisha na tuma fomu kwa barua. Ili kupata maelezo zaidi, bofya ***https://www.ridemetro.org/Pages/FareStudent.aspx***.

## UNAPOKUWA MKAAZI MPYA KWENYE SHULE NCHINI MAREKANI...

### Mazoea na Matarajio

Mazoea, mifumo na maadili ya shule nzima yanakuza tamaduni ya shule inayokuza mahusiano imara na mazingira chanya ya mafunzo. Si sana kuhusu kutii kanuni bali ni zaidi kuhusu kuunda mazingira yanayothaminiwa na kila mtu.

Mifano ya mazoea ya shule na matarajio ya elimu ni:

- Kufuata ratiba na kuzungukia madarasa au walimu
- Darasa zinazojumuisha wasichana na wavulana
- Kuinua mkono ili kuongea
- Cha kufanya wakati wa majaribio ya dharura
- Kurekebisha tabia kwenye muktadha wa shule
- Kupanga foleni ili kuondoka darasani
- Kuvaa au kutovaa sare ya shule
- Umuhimu wa kuhudhuria shuleni na gredi za kadi ya ripoti
- Kufanya kazi kihuria na/au kwa ukimya
- Kuketi tuli kwa vipindi vya muda (huenda vikatofautiana, lakini mara nyingi baina ya darasa za dakika 30-hadi-90)
- Kubadilisha nguo kwa darasa za mafunzo ya mazoezi kwenye chumba cha makabati ya shule
- Kazi za waajiriwa wa shule na yule wa kufuatwa unapokuwa na wasiwasi maalum
- Jinsi wanafunzi na wazazi wanavyohusiana na, na wanavyoingiliana, baina yao

Kufanya kila siku itabirike na izoeke vile unavyoweza. Kufuata ratiba sawia kabla na baada ya shule. Inaweza kuwa kama hivi: Kuamka, kuosha uso, kula kiamshakinywa, kuvaa nguo, kupiga mswaki, kuenda shuleni au kujiunga na darasa mtandaoni. Kupanga ndio ufunguo wa kuwa na siku murwa!

### Bridging Refugee Youth & Children's Services.

Kuwakaribisha na Kuwatanguliza Wanafunzi Wapya Kwenye Shule Nchini Marekani.

Ilichukuliwa Disemba 9, 2020,kutoka kwenye ***https://brycs.org/schools/welcoming-and-orienting-newcomer-students-to-u-s-schools/***

## KUSAIDIA WANAFUNZI WA KIINGEREZA HAPA TX

### Visaidizi vya Houston ISD - *https://www.houstonisd.org/Page/184314*

Orodha ya nyudhuru za kilugha

### Student Digital Resources (Nyenzo za Dijitali za Wanafunzi)

- Imagine Language and Literacy (Uwezo wa Kusoma na Lugha ya Imagine)
- Inajumuisha nyenzo zisizokuwa dijitali za lugha 6 tofauti -- Kiurdu, Kiswahili, Kipoli, Kikareni, Kifursi, Kibama ***http://bit.ly/3osYYf5***

### Nyenzo za Wazazi

### Visaidizi vya Texas Education Agency

Kuwaaidia Wanafunzi wa Kiingereza hapa Texas - ***http://bit.ly/3t69k8k***

Jaza ***Udadisi wa Wazazi na Familia*** ili kuipatia TEA maoni yako, ili wakala na wilaya iweze kukusaidia wewe na watoto wako kwa njia bora zaidi.

## KULEA MTOTO ANAYEONGEA LUGHA MBILI

# Jinsi Jimbo Linavyofuatilia Mwendeleo wa Lugha wa English Learner

Texas English Language Proficiency Assessment System (Mfumo wa Kutahini Ustadi wa Lugha ya Kiingereza wa Texas) (TELPAS) ni mtihani wa kila mwaka kwa wanafunzi kwenye shule za umma za Texas ambao wanajifunza lugha ya Kiingereza. Inatathmini mwendeleo ambao kila EL ameufanya kwenye nyanja nne: kusikiliza, kuongea, kusoma, na kuandika ili kuwa stadi kwenye kutumia Kiingereza cha kimasomo.

Ili wanafunzi watimize uwezo wao wa kimasomo, ni muhimu kwao kufanya mwendeleo imara wa kujifunza Kiingereza. Hapo chini unaweza kupata shughuli kiasi zinazopendekezwa na Texas Education Agency (TEA) ambazo zinaweza kumsaidia mtoto wako ajitayarishe kwa TELPAS.

- Kuunda mazingira yenye fasihi mseto
- Kusoma pamoja au kihuria
- Kusikiliza vitabu vya sauti na kuongea kuhusu mandhari, vibambo, au sehemu bora za kitabu.
- Kuandika kila siku.
- Kutoa Hadithi
- Kuongea Kila Siku



Ili kupata maelezo zaidi kuhusu jinsi ya kutekeleza shughuli hizi, tafadhali fikia kiungo kifuatacho:

Kiingereza: ***https://bit.ly/3clsG3q*** Kihispani: ***https://bit.ly/3iWMHOU***

## HEROD ELEMENTARY SCHOOL (SHULE YA MSINGI YA HEROD)

Siku hizi, kuongea lugha mbili, kusoma lugha mbili, na kuwa na tamaduni mbili ni ndoto ya karibu kila mzazi kuhusiana na watoto wao. Kwenye ulimwengu unaoendelea kubadilika na kustawi, kuweza kuwasiliana kwa lugha kadhaa si uhodari tu, lakini ni tuzo inayoendelea kunufaisha. Unapokuwa unaongea lugha mbili (au lugha kadhaa) fursa zinazokuwa wazi kwako hazina kikomo; kwa hivyo, kumpatia mtoto wako uwezo wa kuongea vizuri angalau lugha mbili kuanzia utotoni ni njia bora kabisa ya kuhakikisha wanafaulu maishani.




**Wanaofurahia Maadhimisho ya Lugha Mbili ya Mwaka wa 25 ni Familia ya Hidalgo. Watoto wao, Kristel Hidalgo *(wa 3)* na Joel Hidalgo *(wa 2)* wanafurahia kuhudhuria kampasi ya Pioneer DL ya HISD. Familia ina matumaini ya kufuatilia manufaa ya kimasomo ambayo Dual Language inawapatia wasomi wao.**

Unapozingatia kauli ya ari ya Herod Elementary School kwenye HISD unaelewa kuwa hii ni hasa kile ambacho walimu na wasimamizi hapo Herod wamejitolea ili kufanya, "Hapa Gary L. Herod Elementary School, ni ari yetu kujitahidi kama jamii shughulishi ili kuwapatia mazingira tulivu ya mafunzo ambapo wanafunzi wote wanahimizwa watimize uwezo wao kamili wa kijamii, kihisia na kimasomo."

Baada ya miaka 25 ya kufungua Mpango wa Lugha Mbili wa kwanza kwenye HISD, Herod ES inaendelea kutoa fursa murwa ya kuongea lugha mbili ili kuwasaidia watoto watimize uwezo wao kamili. Hii ndio sababu kwa nini tungependa kukiri jitihada na bidii isiyochosha ambayo wakufunzi pamoja na jamii nzima ya wazazi, wanafunzi, na wasimamizi wamekuwa wanaitimiza kwa kuwahami wanafunzi kwa zana na uhodari unaohitajika ili kuwa raia wanaoongea lugha mbili, wanaosoma lugha mbili na wenye tamaduni mbili ambao wanahudumia jamii, jumuiya, na ulimwengu wao.

Asante, familia ya Herod, kwa kuendelea kuhimiza wanafunzi wetu wa HISD wawe wanaoongea lugha mbili, wanaosoma lugha mbili, na wenye tamaduni mbili, ili waweze kulipa jamii zao kupitia ufahamu na ustadi wao. Ili kupata maelezo zaidi, tafadhali zuru ***https://www.houstonisd.org/herodelem***

Mwalimu Mkuu: Gina Colión.

Baruapepe: ***gcolionh@houstonisd.org***